International Community of Women Living with HIV Eastern Africa (ICWEA)

## MUHTASARI WA UTAFITI KWA WATUNGAJI SERA

# Kujinaisha Ukimwi
# na athari zake kwa mipango na shughuli za kukabili Ukimwi




## Muktadha wa Sera:

kuhusu kiasi cha faulu au ukosefu wa sera za kitaifa au za kimataifa, masharti na sheria kuhusu suluhisho la Ukimwi. Huibuka kataika muktadha wa Ukimwi na haki za kibinadamu na kuandaa miradi bora ya kukabili Ukimwi. Mkabala bora ni pale unapoweza kutimiza malengo ya jumuiya ya kimataifa ya kupima, kukinga na kutoa matibabu. Mkabala wa Uganda dhidi ya Ukimwi umekuwa wenye uwazi, kuwajibika kwa pamoja, mchango mkubwa wa viongozi wa kisiasa na ushirikiano na mashirika ya nchini na ya kimataifa. Lakini, katika mwaka 2014, nchi ya Uganda ilipitisha sheria ya Kudhibiti na Kukinga Ukimwi. Sehemu III, aya 43 ya sheria hiyo inataja kwamba "yeyote atakayedhamiria au kuwa na nia ya kusambaza Ukimwi kwa mtu mwingine atakuwa ametenda kosa la jinai na atahukumiwa kifungo kinachotimia miaka 10". Tamko hili linachukulia kwamba mtu huwa tayari anajua kuwa ama ana Ukimwi au hana, ndipo "adhamirie" and "awe na nia ya" kusambaza Ukimwi. Lakini, ushahidi wa utafiti uliopo unaonyesha kwamba kitendo kama hiki cha kuchukua hatua za kisheria kinaweza kutia watu hofu wasijitokeze kwenda kupimwa Ukimwi na kupata huduma nyinginezo husika.

# Kujinaisha Ukimwi ni nini?

Kujinaisha Ukimwi ni pale ambapo sheria za jinai zitatumika kwa wagonjwa wa Ukimwi kutokana na hali yao ya kuwa na Ukimwi tu. Hili hutokana na sheria mahususi za jinai, au kutumika kwa sheria za jinai za jumla ambazo zinaruhusu kuhukumiwa kwa mtu aliyemwambukiza mwingine Ukimwi bila kudhamiria, au kushuku kwamba mtu alihatarisha mwingine kumwambukiza Ukimwi wakati mtu huyu hakuambukizwa Ukimwi, au kutomjulisha mchumba kwamba una Ukimwi. Hatua za kujinaisha Ukimwi hazitegemei ushahidi wa utafiti bora wa kisayansi na wa kimatibabu kuhusu Ukimwi. Zinashindwa kushikilia kanuni za haki na usawa wa kisheria (pamoja na kanuni za sheria za jinai zinazohusu sifa za kitendo kinachovunja sheria, kutabiri matokeo ya mbele, dhamira, msababisho, kupima uzito wa kitendo na ushahidi); na hukiuka haki za kibinadamu za wahusika kwenye kesi za jinai. Kulingana na shirika la Haki za Wagonjwa wa Ukimwi, kujinaisha Ukimwi " ni kielelezo cha jinsi serikali inavyoweza kuunga mkono vitendo vya ubaguzi na dhuluma dhidi ya makundi ya watu walio hatarini na kisicho na sifa za kubadilika". Isitoshe, "…kwa kuwa ni kitendo kinachokiuka haki za kibinadamu duniani kote, kujinaisha Ukimwi ni kikwazo kwa watu wote katika upatikanaji wa kinga dhidi ya Ukimwi, kupima, kutoa matibabu na kuuguza wagonjwa wa Ukimwi". Hatua hii inachukuliwa kuwa inabagua kwa kuwa wagonjwa wengine, kwa mfano, wa Kifua Kikuu (TB), magonjwa ya zinaa na mengine hayajinaishwi, mtu anapomwambukiza mwingine[1].

# Kujinaisha uambukizaji Ukimwi au kuhatarisha mtu kupata Ukimwi barani Afrika:

Idadi kubwa ya nchi za barani Afrika zinataja kuambukiza au kuhatarisha mtu kupata Ukimwi kuwa kosa la jinai katika sheria zake kuhusu Ukimwi. Idadi ndogo kutoka nchi hizi zimegeuza sheria za jinai ili kuunda sheria mahususi za kujinaisha kuambukiza Ukimwi au zinazohusu magonjwa ya zinaa. Nchi kutoka Afrika Mashariki ambazo zimeanza kutekeleza sheria zinazojinaisha kuambukiza Ukimwi kwenye sheria zake mpya ni pamoja na Burundi, Kenya, Rwanda, Tanzania na Uganda[2]. Sehemu 171 ya sheria ya jinai ya tamko 120 inataja kwamba " Mtu yeyote, kwa kupuuza au kutotilia maanani, atendaye kitendo ambacho yeye mwenyewe anajua kuwa huenda kikasambaza ugonjwa wowote wa hatari kwa maisha ya binadamu huwa amevunja sheria na atahukumiwa kifungo cha miaka saba'. Nchini Uganda, sheria saba zinazojinaisha uambukizaji Ukimwi ziliundwa kulingana na hali husika, yaani kushitaki kwa ulaghai na bila ushahidi wa msingi ulioandikwa, kuharakisha hukumu bila utaratibu wa upelelezi wa kutosha, hadithi zichapishwazo na vyombo vya habari zinazoendesha ubaguzi, kuvunjika kwa uhusiano wa kimapenzi, maoni ya jamii kuathiri uamuzi wa mahakama; na idadi kubwa zaidi ya wanaoathiriwa ni wasichana

Udadisi wa kesi za wagonjwa uliofanywa na Shirika la haki za Wagonjwa wa Ukimwi, ambapo ama sheria ya jinai au sheria nyingine inayohusiana nayo inatumika kwa wagonjwa wa Ukimwi kwa misingi ya wao kuwa na Ukimwi umeonyesha kuwepo kwa sheria mahususi za kujinaisha Ukimwi katika nchi 29, sheria za jinai za jumla katika nchi 37, au zote mbili (sheria mahususi ya kujinaisha Ukimwi na sheria ya jumla) katika nchi 6. Sheria za aina hii zinajinaisha kutomjulisha wako kuwa una Ukimwi, kushuku kwamba umehatarisha mtu kuambukizwa Ukimwi, au kuambukiza mtu Ukimwi. Mtazamo wa haki za kibinadamu unaonyesha hatari za ubaguzi na kutenga watu ambavyo hutokea sana pale wagonjwa wanapodhulumiwa. Jambo hili ni la muhimu, kwani

1 https://www.aidsmap.com/news/jun-2019/hiv-criminalisation
2 https://hivlawcommission.org/wp-content/uploads/2017/06/Africa-RIB-Criminalisation.pdf

unyanyasaji wa makundi ya watu kama wagonjwa wa Ukimwi, makabila madogo, washogi, watumiaji madawa ya kulevya, na watu wenye ulemavu hutendeka sana katika vituo vya afya. Unyanyasaji huo kawaida hulingana na kuyaona haya makundi kama watu wenye maisha yaliyokiuka kaida au wanaohitaji matibabu ya kipekee ndipo wapone, na kusababisha unyanyasaji tele katika hospitali za matibabu ya kiakili/kisaikolojia, vituo vya kukarabati watumiaji madawa ya kulevya, majela ya makahaba, na mazingira mengine[3]. Aidha, ushahidi unaonyesha kwamba endapo hakuna heshima ya haki za kibinadamu na ubaguzi kwa wagonjwa wa Ukimwi (kama vile kujinaisha Ukimwi), hatua za kukinga dhidi ya Ukimwi zitakwama. Uhusiano kati ya Ukimwi na haki za kibinadamu na jinsi kutokuwepo kwa haki za kibinadamu huathiri harakati za kukinga unabainishwa katika nyanja tatu: Ongezeko la kuhatarishwa (makundi fulani ya watu mkiwemo wanawake na wasichana wako hatarini zaidi kuambukizwa Ukimwi kwa sababu hawana uwezo wa kufurahia haki zao za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni). Ubaguzi na dhuluma: (Haki za wagonjwa wa Ukimwi huvunjwa wakati mwingi kwa kuwashuku au kujua kwamba wao wana Ukimwi, hali inayowaletea kuelemewa na mzigo wa ugonjwa wenyewe na pia kukandamizwa kwa haki zao nyinginezo), na la tatu, hukwamisha kiasi cha faulu cha hatua za kukumbana na Ukimwi: (mikakati ya kukumbana na Ukimwi hukwama katika mazingira ambamo hakuna heshima ya haki za kibinadamu).[4]


Kwa hiyo, lengo la muhtasari huu kwa watungaji sera ni kujenga mtandao na idara za serikali zinazounga mkono utekelezaji wa sera ili harakati za kukumbana na Ukimwi ziungwe mkono na kusawazishwa ipasavyo na shughuli za sera za Serikali ambazo hazionekani kama zinabagua, kudhalimu na kutozingatia hitilafu za kijinsia ndipo kupatikane eneo la Mashariki ya Afrika lililoepukana na ugonjwa wa Ukimwi.

# Udhaifu katika sera na athari zake

**Hitilafu kati ya sera na utekelezaji wake na mapengo katika utekelezaj:** Ingawa sera zimetungwa, baadhi ya sera hizo hazizingatii hali zote; na isitoshe, bado kuna shida ya kutozitekeleza ipasavyo. Miongozo ya kimataifa kuhusu Ukimwi na haki za kibinadamu ya Idara ya Ukimwi ya shirika la Umoja wa Dunia (UNAIDS) ya mwaka 2006, hasa mwongozo namba 4 unataja kwamba “kutunga sera za kijinai na/au za afya ya jamii kusizingatie makosa mahususi dhidi ya kudhamiria kusambaza Ukimwi, bali zinafaa kutumia sheria za jumla za kijinai kwenye kesi hizi za kipekee”. Muhtasari wa utafiti wa Kujinaisha Ukimwi kwa watungaji sera wa idara za Umoja wa Mataifa za UNAIDS na UNDP unataja kwamba “Kushitaki watu mahakamani kutendeke tu kwenye kesi za kudhamiria kusambaza Ugonjwa ambapo mtu fulani alijua kwamba ana Ukimwi, na akatenda kwa madhumuni ya kuambukiza mtu mwingine Ukimwi hadi akafaulu katika kutekeleza lengo hilo. Mtu asishitakiwe mahakamani kama hakukuwa na hatari kubwa ya kusambaza Ukimwi au pale ambapo mtu huyu hakujua kuwa alikuwa na Ukimwi au la, hakuelewa namna ugonjwa wa Ukimwi unavyosambazwa, alimjulisha mchumba wake kwamba ana Ukimwi, hakumjulisha mchumba kwa sababu alikuwa na hofu”.

Kujinaisha usambazaji Ukimwi kunatajwa chini ya Ibara 41 na 43 (Sheria ya kukinga na kudhibiti Ukimwi ya 2014) nchini Uganda kuhusu kujaribu kuambukiza na kudhamiria kuambukiza Ukimwi. Aya 41 inataja kwamba “Mtu yeyote atakayejaribu kusambaza Ukimwi kwa mtu mwingine huwa ametenda kosa la jinai na atahukumiwa kulipa faini isiyozidi shilingi za Uganda laki mbili na arobaine elfu (240,000/=) au kifungo kisichozidi miaka 5 au adhabu zote mbili. Aya 43 inataja

3 https://www.hhrjournal.org/2013/12/human-rights-in-patient-care
4 https://www.ohchr.org/EN/Issues/HIV/Pages/HIVIndex.aspx


Dolutegravir/Lamivudine/
Tenofovir Disoproxil Fumarate
ACRIPTEGA
50 mg/300 mg/300 mg
30 Tablets/Comprimés
Mylan
Cipla
B.No.QK81342
MFD.09/2018
EXP.08/2020
Lopinavir/
Ritonavir
Tablets USP/
Comprimés USP
200 mg /50 mg
POM
GOVERNMENT OF UGANDA
NOT FOR SALE
120 Tablets/Comprimés
Mylan.com
Mylan

kwamba "mtu anayedhamiria au kuchagua kumwambukiza mwingine Ukimwi huwa ametenda kosa la jinai, na akifikishwa mahakamani ataadhibiwa faini isiyozidi shilingi za Uganda miliyoni mbili na laki nne au kupewa kifungo kisichozidi miaka 10 au kupewa adhabu zote mbili". Haya yanapinga Miongozo ya Kimataifa kuhusu Ukimwi, ambayo inapinga sheria mahususi na badala yake inaunga mkono utumikaji wa sheria za jumla za jinai, kwa mfano Aya 171 ya Sheria ya Jinai kwa kesi za mtu kudhamiria kuambukiza Ukimwi kwa mwingine. Mwongozo 4 (21) (a) kuhusu Sheria za Kijinai na Mifumo ya Kukarabati wafungwa inataja kwamba "…utungaji sheria za jinai na za afya ya jamii zisizingatie kesi mahususi dhidi ya uambukizaji Ukimwi kwa dhamira, bali sheria za jumla za jinai zitumike kwenye kesi hizi za kipekee".

**Kutofaulu katika kusababisha kufutwa kwa sheria zilizopo:** Miongozo ya Kimataifa kuhusu Ukimwi na haki za kibinadamu inataja kwamba utumikaji wa sheria ya jinai uwe kwa kiwango kidogo sana. Licha ya haya, kumekuwa na mfumko wa sheria za Ukimwi zinazojinaisha kazi nyingi mbalimbali zinazotendwa na wagonjwa wa Ukimwi. Tangu mwaka 2008, harakati za kupigania usitishaji au ukomeshaji wa utekelezaji wa sheria za kujinaisha kusambaza Ukimwi au kuhatarisha mtu kupata Ukimwi zimepata nguvu mpya. Lakini, jitihada hizi zimekuwa na athari ndogo sana katika kusababisha kufutwa kwa sheria  zilizopo au kusimamisha hatua za serikali za kuanzisha sheria mpya za aina hiyo.

**Kufasili vibaya sheria ya kudhamiria kusambaza Ukimwi:** Wakati mwingi, sheria hizi huwa zimeandikwa vibaya bila maelezo wazi ya kisheria  kuhusu aina ya masharti zinayoweka. Kwa mfano, malalamiko yaliandikwa kutoka Kenya na kutumwa kwa Ofisi ya Kieneo ya Afrika ya Kamisheni ya Dunia ya Ukimwi na Sheria kuhusu fasili ya sharia ya kudhamiria kusambaza Ukimwi. Nchi chache sana barani Afrika zimefuata mwongozo kuhusu Ukimwi na sheria ya jinai katika miongozo ya Kimataifa kuhusu Ukimwi na Haki za Kibinadamu. Badala yake, kumeibuka mfumko wa sheria mpya za Ukimwi ambazo zinajinaisha kazi mbalimbali za watu wenye Ukimwi kutoka kudhamiria kuambukiza mtu mwingine Ukimwi hadi kuficha mchumba wako kuwa una Ukimwi.

**Ongezeko la kuhatarishwa:** Baadhi ya makundi ya watu wako hatarini zaidi kuambukizwa Ukimwi kwa sababu hawana uwezo wa kutenda haki zao za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Kwa mfano, watu binafsi wanaonyimwa haki ya kujiunga na vikundi na kupata habari wataanchwa nje ya mijadala kuhusu Ukimwi, kushiriki kwenye mashirika yatoayo huduma za Ukimwi, na makundi yenye miradi ya kujiendeleza, au kuzingatia njia nyinginezo za kujikinga na kujilinda wasiambukizwe Ukimwi.

**Ubaguzi na kutengwa:** Haki za watu wenye Ukimwi huvunjwa wakati mwingi kwa sababu ya kushukiwa au kujua kwamba wana Ukimwi, na kusababisha kuelemewa mzigo wa ugonjwa wenyewe na athari zake za kupoteza haki nyinginezo. Kudhulumiwa na kubaguliwa  vinaweza kuzuia upatikanaji wa matibabu kwao na huweza kuathiri kazi zao, maskani yao na haki nyinginezo. Hali hii kisha huchangia uhatarishaji wa watu wengine kuambukizwa Ukimwi kwa kuwa dhuluma na ubaguzi vinavyohusiana na Ukimwi huvunja moyo wa wagonjwa wa Ukimwi wasiende kupata huduma za kiafya na za kijamii. Watu wanapopuuza huduma za Ukimwi na habari kuhusu Ukimwi au matibabu, na huduma za matibabu na kuuguza, huzidisha kusambaa kwa ugonjwa wa Ukimwi. Vipengele hivi ni vya muhimu sana katika harakati bora za kukumbana na Ukimwi. Kuweka mazingira hasi kwa wagonjwa wa Ukimwi, na vizuizi vingine vinavyohusiana na kupima Ukimwi, matibabu na mtu kutangazia mchumba wake kuwa ana Ukimwi huwahatarisha zaidi kutendewa vitendo vya uhasama.

## Hitimisho

Utungaji sheria kote Afrika Mashariki haujategemea ushahidi mpya wa kisayansi. Wakati mwingi, dhamira ya mgongwa haihitajiki na lengo la kushitaki mtu limelenga tabia ya mtu kutotilia maanani. Hakuna Ushahidi kwamba sheria hizi zimekuwa na kiasi chochote cha faulu katika kuzuia usambazaji Ukimwi. Sheria za nchi zinakiuka kanuni za kimataifa za haki za kibinadamu ijapo kuwa zilitungwa baada ya ushahidi kutoka sehemu nyinigezo za dunia kuonyesha kwamba kujinaisha Ukimwi hakupunguzi kiasi cha usambazaji wa virusi vya Ukimwi. Sheria hizi zinadhihirisha udhaifu katika kusuluhisha chanzo chenyewe cha dhuluma na ubaguzi. Sheria hizi pia zinashindwa kuonyesha wajibu wa jamii nzima kukinga watu wapya dhidi ya kuambukizwa Ukimwi. Kwa hiyo, ili kuboresha suluhisho la Ukimwi na haki za wagonjwa wa Ukimwi, nchi zinafaa kushirikiana, kusawazisha mazingira ya sera na kutekeleza masuluhisho ambayo yanaheshimu haki za wagonjwa wa Ukimwi na pia kuzingatia changamoto za kipekee za makundi maalum ya watu kama vile wanawake wenye Ukimwi. Masuluhisho kutoka serikali na pia mashirika yatowayo usaidizi yaungwe mkono na mfumo wa sera unaochangia upatikanaji wa jamii huru na iliyo wazi na kufaulu kutimiza malengo ya kukabili Ukimwi ya kuwa na dunia isiyo na Ukimwi.

## Mapendekezo kwa watungaji sera ili kuboresha hatua za kukabili Ukimwi na haki za wagonjwa wa Ukimwi

- Mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wengine wafute matamko ya sehemu mbalimbali za sheria za nchi za Afrika Mashariki ambazo zinajinaisha usambazaji Ukimwi.
- Matamko mapya ya sera yatoe mazingira ambayo yanawapa motisha watu kwenda kupimwa Ukimwi bila ya hofu kwamba hali yao ya kuwa na Ukimwi itahusishwa na jinai.
- Mafunzo na habari kuhusu Ukimwi yatangulizwe katika huduma zote za afya kuwezesha watu kupata huduma mwafaka wakati wowote kabla ya wao kuhangaika.
- Tofauti za kijinsia zizingatiwe kwenye shughuli zote za utungaji na utekelezaji wa sera za Ukimwi kwa sababu ya changamoto za kipekee ambazo wanawake wanakumbana nazo maishani ili kusuluhisha hitilafu zilizopo katika kupata huduma na kupunguza mkondo wa maambukizi mapya ya Ukimwi ambayo yanaathiri hasa wanawake.

### FOR MORE INFORMATION

The International Community of Women Living with HIV Eastern Africa (ICWEA)
Plot 1106, Ssenge - Kawanda Road,
Off Kayunga Kampala - Hoima Road,
P.O. Box 32252, Kampala, Uganda
Tel. +256 414531913 Mobile: +256392947313
Email: admin@icwea.org Twitter: @ICWEastAfrica
Facebook: ICW Eastern Africa
Website: www.icwea.org

AFRICAN WOMEN'S DEVELOPMENT FUND